November 2016 subject reports

# Swahili B

## Overall grade boundaries

### Higher level

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 14 | 15 - 26 | 27 - 42 | 43 - 56 | 57 - 69 | 70 - 83 | 84 - 100 |

### Standard level

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 12 | 13 - 25 | 26 - 43 | 44 - 59 | 60 - 73 | 74 - 85 | 86 - 100 |

## Higher level internal assessment

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 12 | 13 - 17 | 18 - 21 | 22 - 26 | 27 - 30 |

As there were very few candidates entered for HL this session, it is inappropriate to draw conclusions on candidate performance.

## Standard level internal assessment

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 12 | 13 - 17 | 18 - 21 | 22 - 26 | 27 - 30 |

## Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Mada zilizowasilishwa pamoja kutumia picha zilikuwa za kufaa. Walimu walijumuisha mada tofauti zilizoambatana na picha mbalimbali pamoja na maandishi yaliyofuata chini ya kila picha. Maandishi katika kila picha yalikuwa na jukumu la kuwa kichocheo kizuri ili mwanafunzi apate mwelekeo anapowasilisha. Walimu waliongoza mawasilisho kwa utaratibu mzuri; kila mwanafunzi alikuwa na muda wa kutosha kuwasilisha na kushiriki katika sehemu ya maswali. Kwa kiasi kikubwa, walimu waliweza kuwauliza wanafunzi maswali ambayo yaliwawezesha wanafunzi kupanua mawanda yao kifikira na katika matumizi ya lugha. Mawasilisho haya yaliwasaidia wanafunzi kuwa wabunifu katika matumizi ya lugha ili kujadili dhana tofauti. Wanafunzi pamoja na walimu walifuata maagizo na kuyatekeleza ifaavyo kulingana na kanuni za zoezi hili. Ubora wa sauti zilizorekodiwa ulikuwa wa hali ya juu na muda ulizingatiwa katika sehemu zote mbili.

## Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Kwa jumla, watahiniwa wengi walikuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya zoezi hili. Watahiniwa walifahamu jinsi ya kutekeleza zoezi hili na kufuata maagizo yaliyotarajiwa. Katika kigezo A, wanafunzi walidhihirisha uelewa mzuri na waliweza kueleza picha wakizihusisha na mandishi yaliyofuata. Isipokuwa matatizo ya madogo ya kisarufi, mawasilisho yalieleweka kwa njia nzuri.

Ni katika sehemu ya majadiliano wanafunzi wengi walikuwa wanasitasita wanapoongea huku wengine wakinyamaza kwa muda kabla ya kupata maneno ya kujadili mawazo kulingana na maswali ya walimu. Huenda ikawa ni woga wa kujibu maswali yanayoulizwa bila kutarajia. Wengine walikuwa wanapotoka kulingana na maswali yaliyoulizwa, lakini walimu walifanya hima kufafanua zaidi maswali hayo. Idadi kubwa ya watahiniwa iliweza kudumisha mazungumzo baina yao na walimu. Matamshi yalikuwa sawa na lafudhi za wanafunzi walipokuwa wanawasilisha hazikutatiza mawasiliano.

Kwa jumla, wanafunzi waliweza kuzizungumzia picha walizopatiwa kwa urahisi kuliko walivyoshiriki katika sehemu ya pili ya mazungumzo.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Kuna wanafunzi ambao walitumia zaidi ya dakika nne walipowasilisha na hivyo hawakuwa na muda wa kutosha katika sehemu ya mazungumzo. Pia, kuna wale waliotumia muda zaidi kuelezea picha na kupunguza muda wa maswali kwa kiasi kikubwa. Ingewezekana, ni vyema kufanya mazoezi ya zoezi hili mara nyingi iwezekanavyo ili wazoee. Ningependekeza pia wawekewe saa darasani na wanapowasilisha wawe wanaangalia wametumia muda gani na wamebakisha dakika ngapi. Pendekezo lingiine ni kwa walimu kuhakikisha maswali wanayoyauliza katika sehemu ya mazungumzo yana uwazi. Ufafanuzi wa maswali mtahiniwa asipoelewa vizuri ni muhimu ali aweze kuyajibu. Hata walimu wazingatie muda na wasiwaharikishe wanafunzi kabla ya muda wao kuisha. Maswali yanayohusu majibu ya moja kwa moja yanafaa yaepukwe; kwa mfano swali linalomhitaji mwanafunzi kusema jina la mwanasiasa au kiongozi wa upinzani na chama cha kikuu cha upinzani. Ningependekeza swali/ maswali yanayoweza kuibua jibu/majibu ambayo yatahitaji mtahiniwa kutoa maoni yake kuhusu jambo fulani, au maswali ambayo yatahusisha matumizi ya lugha. Wala si maswali yanayohitaji neno moja au ‘ndiyo/la’ kama jibu

## Maoni mengine

Walimu pamoja na wanafunzi walihusika vizuri kuhakikisha zoezi hili limefaulu. Kwa wale wanafunzi wanaoishiwa na hoja na kunyamaza kwa kuda, ni vyema mwalimu kujaribu kuuliza swali lile kwa njia nyingine au kufafanua zaidi ili kumwezesha mwanafnzi kuendeleza mazungumzo; hasa katika sehemu ya pili. Ni vizuri pia kuepuka mtindo wa ‘swali-jibu’ kutoka mwanzo hadi mwisho wa mazungumzo. Jambo lingine ni mwalimu kuishiwa na maswali. Kuna tukio ambalo mwalimu aligundua kuwa bado kulikuwa na muda baada ya kutoa ishara kwa mwanafunzi muda umeyoyoma. Ili kuhakikisha muda wote umetumika maswali yaliyofuata hayakuwa yanapima uwezo wa lugha hata kidogo, bali kupitisha muda.

Jambo lingine ambalo ningependekeza ni kuepuka maandshi ambayo ni marefu sana. Hata hivyo, mawasilisho yote yaliandamana na picha zilizokuwa wazi na zilizokuwa zinaeleweka kwani zilikuwa ni picha zinazotoa uhalisia unaoeleweka katika maisha ya wanafunzi. Picha nyingi zilikuwa za kuvutia na za kuteka mawazo ya wanafunzi kwa njia nzuri.

## Higher level written assignment

### Component grade boundaries

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| **Mark range:** | 0 - 4 | 5 - 8 | 9 - 12 | 13 - 15 | 16 - 17 | 18 - 20 | 21 - 24 |

As there were very few candidates entered for HL this session, it is inappropriate to draw conclusions on candidate performance.

# Standard level written assignment

## Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 7 | 8 - 11 | 12 - 14 | 15 - 17 | 18 - 20 | 21 - 24 |

# Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Watahiniwa walifahamu na kufuata kanuni kulingana na maagizo. Kwa kuwa wanafunzi walikuwa na uhuru wa kujichagulia mada zao, wengi waliweza kutimiza mahitaji ya kazi hii na kuandika kuhusu mada kama walivyozitanguliza. Kuwapa wanafunzi fursa ya kuandika kazi zao wakirejelea vyanzo mbalimbali ambazo walizisoma kabla ya kuandika ni njia nzuri ya kuwatayarisha vizuri kuandika kazi za utafiti katika ngazi nyingine za masomo kama vile vyuo vikuu. Uhuru wa kuchagua mada na marejeleo ni njia nzuri pia ya kuwawezesha kuandika bila kufungika katika mada fulani. Wanafunzi pia walipata nafasi ya kutalii tanzu mbalimbali za uandishi kama vile baruapepe, hotuba, mahojiano na kadhalika. Kwa njia hii, waliweza kutumia njia walizochagua wenyewe kuwasilisha ujumbe bila kuhitajika kuandika kwa kutumia mtindo fulani. Kazi nyingi zilizowasilishwa zilikuwa zimefuata utaratibu unaofaa.

# Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Wanafunzi walifikisha ujumbe wao kwa njia mbalimbali, kama vile, barua, hotuba, mahojiano na kadhalika. Malengo ya kila kazi yalikuwa yameelezwa vizuri katika utangulizi. Isipokuwa wachache, wengi waliweza kutumia mpangilio na muundo unaofaa kwa kila tanzu la uandishi. Kwa nadra sana watahiniwa walidokeza kutumia njia fulani ya uandishi na kisha kupotoka walipofikia katika kuandika kazi yenyewe. Hata hivyo, kuna mmoja aliyeandika makala iliyoachambua kazi ya kifasihi, kinyume na matakwa ya zoezi hili. Kwa upande wa lugha, wengi walionyesha uwezo wa hali ya juu ingawa kuna wale waliokuwa na matatizo ya kisarufi. Uandishi wa kazi kulingana na mada na kama ilivyotangulizwa ulikuwa wa kufaa. Watahiniwa walikuwa na uwezo mzuri wa kukuza hoja zao na kuzipangilia kwa njia mwafaka. Tatizo lililojitokeza ingawa si kwa kiasi kikubwa ni uwezo wa kueleza marejeleo au vyanzo vya kazi mbalimbali katika utangulizi wa kazi. Baadhi walitaja mada za vyanzo vyao bila kuvieleza, wengine walivitaja na kuvieleza kama chanzo kimoja, ilhali wengine hawakuvitaja hata kidogo. Katika uandishi wa kazi yenyewe, wengi walionyesha ustadi wa hali ya juu. Kuna mmoja au wawili walioandika kazi zao kana kwamba wanayachambua makala ambayo walikuwa wamerejelea badala ya kujenga ubunifu wao kuegemea makala hizo. Kwa jumla, hakuna kigezo fulani kinaweza kusemekana kuwa watahiniwa walikuwa na changamoto hasa.



International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Cha muhimu ni wanafunzi kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili kupata uzoefu na kujua ni nini kinahitajika. Ni vyema wanafunzi wafanye mazoezi ya kueleza vyanzo vya kazi zao. Kwa sababu kuna wale ambao hawakueleza vyanzo vyao wala kuvitaja. Jambo lingine ni walimu kuwahimiza wanafunzi wachague mada ambazo wataweza kuziandikia na tena mada zile watakuwa na urahisi wa kupata marejeleo. Ni vizuri kuzikagua kazi za watahiniwa vizuri. Ningependekeza hata walimu wazipitie kanuni na mahitaji ya kazi hii ili kuepuka tukio la watahiniwa kutofuata maagizo

## Maoni mengine

Kazi ya aina hii ni nzuri kwa sababu inawawezesha wanafunzi kutumia makala tofauti na kukuza ubunifu wao kwa kuandika kazi moja inayohusisha makala hizo. Wanafunzi kwa jumla walikuwa wamejiandaa vizuri, na walimu walikuwa wamewatayarisha kwa kazi hii ipasavyo.

## Higher level paper one

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 12 | 13 - 19 | 20 - 27 | 28 - 34 | 35 - 41 | 42 - 47 | 48 - 60 |

As there were very few candidates entered for HL this session, it is inappropriate to draw conclusions on candidate performance.

## Standard level paper one

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 6 | 7 - 13 | 14 - 20 | 21 - 27 | 28 - 35 | 36 - 40 | 41 - 45 |

## Maoni ya jumla

Mtihani huu ulikuwa wa kufaa kiwango hiki. Vifungu vyote vilikuwa vinaeleweka na maswali yalikuwa wazi. Matokeo ya mtihani yalikuwa ya mtindo wa kawaida; kuna waliopata alama za juu zaidi, wastani, na za chini. Aina tofauti za maswali zilijumuishwa katika mtihani huu ili


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional

kuwapa wanafunzi fursa mbalimbali na kutahini uwezo wao katika viwango tofauti: sarufi, ufahamu, msamiati na kadhalika.

## Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Ugumu wa maswali haukupatikana katika aina fulani ya maswali hasa. Hii ni kwa sababu wanafunzi walikuwa na uwezo katika maswali fulani huku wakilemewa na maswali ya aina hiyo hiyo katika sehemu nyingine. Hata hivyo kuna maswali mawili ya msamiati (25 na 26) ambayo zaidi ya nusu ya watahiniwa walifeli. Sehemu nyingine iliyowatatiza wanafunzi ni maswali mawili ya kuchagua majibu (28 na 30) katika kifungu C. Haiwezi ikawa dhibitisho kuwa wanafunzi wana ugumu wa kujibu maswali ya msamiatii au ya majibu ya kuchagua; hii ni kwa sababu wanafunzi walifanya vizuri katika sehemu nyingine ambazo maswali ya aina hii yalipatikana. Maswali ya kifungu C yalionekenana kuwa changamoto kwa watahiniwa wengi kuliko shemu nyingine. Aina nyingine ya maswali iliyowatatiza wengi ni sehemu ambayo mtahiniwa alihitajika kuchagua kifungu cha maneno kukamilisha kipande cha sentensi (23) katika upande wa kushoto. Hata hivyo, si maswali yote ya aina hii yaliwatatiza wanafunzi.

## Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Sehemu ambayo wanafunzi walifanya vizuri zaidi ni ya maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika kifungu cha mwisho (38, 39, na 40). Sehemu nyingine ni ya maswali ya kuchagua majibu katika kifungu hicho cha mwisho. Maswali ya msamiati katika kifundu A pia hayakuwatatiza wengi. Kwa jumla, Maswali ya kifungu D yalikuwa rahisi kwa watahiniwa wengi, ilhali ya kifungu C yalikuwa changamoto kwa wengi. Maswali ya vifungu A and B yalikuwa na ugumu wa wastani. Maswali ambayo yalihitaji majibu mafupi kunakiliwa kutoka kwenye kifungu yalikuwa ya wastani, kuna yale wanafunzi wengi waliyapata na kuna yale wengi walifeli.

## Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Kila mtahiniwa alikuwa na uwezo wake tofauti kwa maswali binafsi. Asilimia kubwa ya watahiniwa ilidhihirisha uelewa wa vifungu vyote na maswali yaliyofuata licha ya wengine kutoa majibu ambayo hayafai. Kufeli maswali yaliyohitaji wanafunzi kuchagua kauli zilizo za kweli kutoka orodha iliyotolewa ni ishara ya kuwa wengi walioanguka maswali haya hawakurejelea kifungu kwa mara nyingine ili kuchunja majibu ambayo hayakuwa na uwezekano wa kuwa sahihi, ingawa wengi walipata majibu sahihi katika sehemu hii. Katika maswali yaliyohitaji wanafunzi kuweka alama ili kuonyesha kama kauli fulani ni ya kweli au si kweli na kisha kutoa thibitisho, wengi walipata maswali haya kuliko mwaka wa 2015. Udhaifu ulioonekana kulemaza uwezo wa kupata majibu ulitokana hasa na kutoelewa swali au kifungu vizuri.

Kuna wale walioandika nukuu ndefu zaidi kiasi cha kukosa kutoshea katika nafasi za majibu walizopatiwa. Hii ni kutokana na kutoelewa swali au kifungu vizuri. Wengine walinukuu sehemu moja ya jibu linalohitajika na kuacha sehemu nyigine ili nukuu iwe kamili na sahihi.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Umuhimu wa kurejelea kifungu mara nyingi iwezekanavyo ni vizuri usisitizwa. Jinsi ya kuchuja majibu ambayo hayana uwezekano wa kuwa sahihi hadi mtahiniwa abaki na jibu lililo sahihi ni mbinu nyingine wanafunzi wanafaa kufundishwa pindi tu wajipatapo katika hali ambayo swali limekuwa ngumu. Manufaa ya kila sehemu ya maswali kutoa maagizo ni aya gani mtahiniwa anafaa kurejelea ili kujibu swali fulani yanafaa kusisitizwa pia. Katika sehemu ya msamiati, ni uzoefu wa lugha tu utakaowawezesha kukabiliana na maswali ya aina hii; hivyo kupendekeza mazoezi zaidi.

## Higher level paper two

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 4 | 5 - 10 | 11 - 16 | 17 - 23 | 24 - 30 | 31 - 37 | 38 - 45 |

As there were very few candidates entered for HL this session, it is inappropriate to draw conclusions on candidate performance.

## Standard level paper two

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 11 | 12 - 15 | 16 - 18 | 19 - 20 | 21 - 25 |

## Maoni ya jumla

Maswali na maagizo katika karatasi hii yalikuwa ya kiwango mwafaka. Ingawa wengi walipendelea kuandika kuhusu mada fulani, hakuna swali lolote lilikosa kujibiwa. Maswali matano katika karatasi hii ni manufaa kwa watahiniwa kwani wanapata nafasi ya kuchagua swali ambalo wana urahisi wa kujibu. Mada tofauti pia ziliwapa wanafunzi nafasi ya kuchagua maswali tofauti. Kwa jumla, wanafunzi walielewa walichotakiwa kufanya na walifuata maagizo ipasavyo ingawa kulikuwa na wachache waliokuwa na changamoto mbalimbali.


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional

## Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Kuna sehemu mbili ambazo wanafunzi walionekana wakizikwepa; sehemu ya mila na desturi na ya afya. Swali lililoangazia suala la afya lilihitaji kuandikiwa insha inayolenga kujadili manufaa na madhara ya dawa za kisasa na dawa mbadala. Huenda swali halikueleweka vizuri ama wanafunzi hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuandikia suala linalohusu aina tofauti za dawa; za kisasa na dawa mbadala.  Swali lingine lililokwepwa na wanafunzi ni swali la mila na desturi ambalo lilihitaji kuandikiwa shajara kuhusu changamoto za kosomea lugha katika mazingira mengine isipokuwa darasani. Huenda ikawa swali halikueleweka vizuri au wanafunzi hawangeweza kubuni hoja mwafaka kuandikia suala hili, au iwe si wengi wanaoelewa mtindo na muundo wa shajara. Swali la burudani lililohusu siku ya michezo shuleni katika makala ya gazeti la shule lilijibiwa na wanafunzi wachache, ambao wengi wao waliandika hoja ambazo zilikuwa zinapotoka kwa kiasi fulani. Huenda swali lenyewe halikueleweka vizuri. Hata hivyo, katika hayo maswali yaliyoonekana kuwa magumu, kuna wanafunzi walioandika insha nzuri na kudhihirisha ubingwa wao wa lugha na uelewa wa maswali na kilichohitajika.

## Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Uandishi wa baruapepe pamoja na hotuba ulichangamkiwa na wanafunzi wengi kuliko aina nyingine za uandishi. Huenda ikawa ni kwa sababu wengi wana mazoea ya kuwaandikia marafiki au jamaa zao baruapepe wakati mwingi. Mada hii ya utofauti wa tamaduni haikuwa inatofautiana sana na mada ya mila na desturi ya swali la pili ambalo wanafunzi walitakiwa kuandika shajara lakini wengi walilikwepa. Mazoea ya kuandika baruapepe kuliko shajara huenda yakawa ndiyo yalisababisha wengi kujibu swali la kwanza la baruapepe. Swali la tano lililokuwa linahusu mada ya sayansi na teknolojia na mada ndogo ya matumizi ya simu miongoni mwa wanafunzi wakiwa shuleni lilijibiwa na watu wengi pia. Swali hili lilikuwa linahitaji kuandikiwa hotuba kupinnga au kuunga mkono marufuku ya simu shuleni. Mara nyingi wanafunzi shuleni hujihusisha na mijadala ya kuunga mkono au kupinga mada fulani na huenda uzoefu huu ndio ulipelekea wanafunzi kulipendelea swali hili. Suala la simu miongoni mwa wanafunizi pia linaeleweka na wengi ambao wanahusika na matumizi ya simu shuleni; na ndio maana walilichangamkia zaidi.

## Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Wanafunzi walionyesha uwezo mkubwa katika swali lililohitaji kuandikiwa baruapepe na lile la hotuba. Urahisi na mazoea ya kuandika baruapepe ni kigezo kilichopelekea wengi kufanya vizuri. Swali la hotuba nalo lilihusu simu za mkononi miongoni mwa wanafunzi na kwa sababu ni jambo wanalokabiliana nalo kila siku, walikuwa na urahisi wa kuliandikia. Wanafunzi pia walionyesha uwezo na uelewa wa mitindo ya uandishi ya kazi mbalimbali; kama vile muundo wa baruapepe, hotuba, insha, na kadhalika. Vipengele kama vile utangulizi, uendelezaji wa kazi, hitimisho/pendekezo ni mambo ambayo yalionekana kuwa yanaeleweka vizuri. Wanafunzi pia walionyesha uelewa wa mada tofauti na kilichokuwa kinahitaji kuandikiwa.

Licha ya kudhihirisha uwezo wao katika ngazi tofauti, kuna matatizo yaliyoonekana miongoni mwa wanafunzi na huenda yalisababisha wengina kutopata alama za juu. Kuna wengine walipotoka katika sehemu mbalimbali za kazi zao na kuandika hoja ambazo hazikuhusiana na maswali kulingana na maagizo. Wengine waliandika mada tofauti kinyume na maagizo kama yalivyotolewa, huku wachache wakitumia mitindo tofauti kinyume na maagizo.

Kuna kazi chache zilizokuwa tatizo kusoma kutokana na miandiko dhaifu.

Kwa wanafunzi wengine, kuna wale walipoteza muda mwingi kuandika nakala chafu kisha kuandika nakala safi. Cha kushangaza ni kuwa kwa wengine hakukuwa na tofauti kati ya nakala chafu na safi. Hii ilipeleka wengine kukosa wakati wa kutosha kuandika nakala safi na kuutumia kuandika nakala chafu.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Mazoezi ya kuandika aina tofauti za insha yatasaidia uzoefu wa wanafunzi katika tanzu mbalimbali za uandishi. Jambo lingine ni wanafunzi kuhimizwa kusoma maagizo kwa makini ili kuweza kujibu maswali kama yanavyohitajika. Ili kuokoa muda wanapoandika nakala chafu na kisha kuandika nakala safi ambayo inatoshana na nakala chafu kwa urefu na kina, ningependekeza wanafunzi wafanye mazoezi ya kuandika vidokezo badala ya kuandika insha ndefu na kisha kuinakili tena. Pia, wanfunzi wanaweza kufundishwa jinsi ya kuandika nakala chafu ambazo ni fupi na hazitumii muda mrefu na kunyima wanafunzi muda wa kutosha kuandika nakala safi.

Miandiko ya wanafunzi ni jambo lingine ambalo wanafunzi wanafaa kuangalia kwa makini. Kazi ambazo ni chafu na miandiko isiyosomeka husababisha maneno mengine kutosomeka kabisa na hivyo kupelekea wanafunzi wenye kazi hizo kutopata alama za juu. Ni vyema wanafunzi waboreshe hati zao.


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional